# *HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA*

## *SHERIA NDOGO ZA ( ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA, 2013*

**TANGAZO LA SERIKALI NAMBA 369 LA TAREHE 3/10/2014**

**SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA, 1982**

***(SURA YA 290)***

**SHERIA NDOGO**

*Zimetungwa chini ya kifungu cha 6 (1) na 16 (1)*

**SHERIA NDOGO ZA(ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA ZA MWAKA, 2013.**

Jina na tarehe ya kuanza kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela za mwaka 2013 na zitaanza kutumika mara baada ya kutangazwa kwenye gazeti la Serikali.

Eneo la kutumika

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililopo chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela.

Tafsri ya maneno

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa kama itahitajika vinginevyo:-
"Afisa Mwidhiniwa" ni mtu yeyote atakayeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi akiwemo.

"Bango" ni tangazo lolote kwa madhumuni ya kibiashara lililo kwenye nyumba au kitu chochote kwa madhumuni ya kutangaza chochote.

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela.

"Madini ya ujenzi" yataambatanisha aina yoyote ya miamba, mawe, kokoto, mchanga, mfinyanzi yatakayotumika kwa shughuli za ujenzi wa majengo, barabara au viwanja mbalimbali.

"Mazao" maana yake ni mazao yote ya chakula, biashara, maua, matunda na mboga yanayolimwa ndani ya Halmashauri.

"Mifugo" maana yake ni wanyama wote wafugwao na binadamu na itajumuisha nyuki, samaki, bata na kuku.

"Mfugaji" maana yake ni mtu yeyote anayejishughulisha na ufugaji wa mifugo katika eneo la Halmashauri.

"Mkazi" maana yake ni raia wa Tanzania ambaye kwa kawaida anaishi kwenye eneo la Halmashauri na ambaye ana kaya au anaishi katika kaya au taasisi iliyopo katika eneo la Halmashauri, isipokua mtu;

(a) mwenye umri chini ya miaka 18;
(b) asiyejiweza kutokana na ulemavu, kuugua au uzee wa zaidi ya miaka sitini ambaye ni tengemezi kwa mtu mwingine;
(c) mwanafunzi aliyeko masomoni muda wote.

"Mkurugenzi" inamaanisha Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilemela au mtu yeyote atakayefanya kazi kwa niaba yake.

"Mwalo" eneo wanaloshushia na kupakia samaki na mizigo mingineyo ambalo linapakana na ziwa.

"Sheria" inamaanisha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura 290.

"Soko" Maana yake ni eneo lolote llilotengwa rasmi na Manispaa kwa matumizi ya soko.

"Wakala" inamaana ya mtu, shirika, taasisi, kampuni au kikundi kilichoteuliwa na kupewa jukumu la kukusanya ushuru chini ya Sheria Ndogo hizi.

Ulipaji wa Ada na Ushuru

4. (1) Italipwa ada na ushuru utakaokusanywa na Manispaa kutoka kwa wafanyabishara kutokana na huduma na vibali vitolewavyo na Halmashauri.

(2) Ada na ushuru vitakavyolipwa kutokana na Sheria ndogo hizi vitalipwa kuanzia tarehe 1 mwezi Julai hadi tarehe 30 Juni ambapo itakuwa siku ya mwisho ya kulipa kodi mbalimbali kwa Halmashauri katika mwaka wa fedha husika.

(3)Mawakala watalipa kadri ya mikataba yao.

Wajibu wa Kulipa Ada na Ushuru

5. Utakuwa wajibu wa kila mtu anayepaswa kulipa ada na ushuru kulipa kwa Afisa Mwidhiniwa au Wakala wa Halmashauri kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.

Ada na ushuru

6. (1) Kutakuwa na ada na ushuru vitakavyotozwa na Halmshauri na kulipwa na kila mfanyabiashara anayefanya biashara ndani ya mamlaka ya Halmshauri. Viwango hivyo vitakuwa kama vinavyoonekana katika sehemu ya pili ya Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Ada na ushuru utozwao chini ya Sheria Ndogo hizi utalipwa kabla ya kupatiwa leseni, kibali au huduma husika na utakuwa kama ilivyoonyeshwa kwenye Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(3) Ada na ushuru vitalipwa kadri vilivyooneshwa sehemu husika katika Jedwali.

(4) Ada na Ushuru vilivyooneshwa katika aya ndogo ya kwanza ya Sheria Ndogo hizi vitatozwa kwa kila mtu atakayepokea huduma au kufanya biashara ndani ya mipaka ya mamlaka ya Halmashauri.

(5) Ada na ushuru unaotozwa na Halmashauri vitalipwa kwa Halmashauri au wakala wake.

Vibali vya matangazo ya biashara

7. (1) Matangazo, alama za matangazo na au kifaa chochote kitakachosimamishwa ndani ya mamlaka ya Halmashauri, kiwe kwenye barabara kubwa au za mitaa, maeneo ya wazi, majengo au eneo lolote kwa lengo la kutangaza biashara, hakitaruhusiwa kuwekwa mpaka maombi na idhini kutolewa na malipo stahili yamelipwa kwa Halmashauri.

(2) Hakuna idhini itakayotolewa kupaka rangi tangazo lolote la biashara kwenye nyumba ya kuishi, mawe au kitu chochote cha asili ndani ya mamlaka ya Halmashauri.

Madini ya ujenzi

8. (1) Migodi midogo ambapo madini ya ujenzi yatachimbwa itakuwa chini ya milki ya Halmshauri.

(2) Halmshauri itatenga maeno maalumu ambapo madini ya ujenzi yatakuwa yanachimbwa kwa madhumuni ya Sheria Ndogo hizi.

(3) Mtu yeyote hatochimba madini ya ujenzi ndani ya mamlaka ya Halmashauri isipokuwa kwa mamlaka na kibali cha Halmshauri.

(4) Mtu yeyote atakayechimba madini ya ujenzi kutoka sehemu nyingine tofauti na maeneo yaliyotengwa rasmi na Halmashauri, atakuwa anafanya kosa na akikutwa na hatia, atatozwa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na miwili au vyote viwili kwa pamoja.

(5) Madini ya ujenzi yatakayopatikana kwa kukiuka Sheria Ndogo hizi, yakikamatwa pamoja na adhabu nyingine yatataifishwa.

Ada na Ushuru wa madini ya ujenzi

9. (1) Utatozwa ada na ushuru wa kuchimba madini ya ujenzi ndani ya mamlaka ya Halmashauri.

(2) Zaidi ya ushuru wa madini ya ujenzi, itatozwa ada ya kibali cha kuchimba madini ya ujenzi kama inavyoelekezwa katika jedwali la kwanza la sheria ndogo.

Ushuru wa bidhaa mbalimbali ndani ya Halmashauri

10. (1) Utatozwa ushuru kwa bidhaa kama zilivyoainishwa kwenye Jedwali la Kwanza.

(2) Mtu yeyote hatonunua au kuuza au kubadilishaana bidhaa au mazao yoyote ndani ya mamlaka ya Halmashauri isipokuwa katika masoko tu.

(3) Kuuza, kununua au kubadilishana bidhaa kunaweza kufanyika nje ya soko kwa idhini na kibali maalumu cha maandishi cha Halmashaauri au endapo kuuza, kununua au kubadilishana bidhaa kuwe kwa ajiri ya matumizi ya nyumbani.

(4) Halmshauri inaweza kuelekeza aina fulani za mazao kuuzwa kwa mnada wa wazi, na kuwa mnada huo utakuwa kadri Halimashauri itakavyoelekeza.

Ushuru wa Samaki

11. (1) Kutakuwa na ushuru wa samaki kama ulivyobainishwa kwenye Jedwali la Kwanza la sheria ndogo hizi.

(2) Ushuru wa samaki utatozwa katika mialo yote iliyo ndani ya mamlaka ya Halmshauri.

(3) Litakuwa jukumu la kila mwenye eneo la ardhi ndani ya mita thelathini kutoka ziwani:-

a) Kutoa taarifa zozote ambazo Halmashauri itataka,
b) Atasaidia Halmashauri kutekeleza majukumu yake ya kutambua masanduku ya samaki pamoja na kutoza ushuru wa mazao ya samaki.

Izingatiwe kuwa, endapo mwenye eneo la uvuvi atakataa kutoa taarifa kwa uwezo wa ufahamu wake, au kwa kujua akatoa taarifa potofu, atakuwa amefanya kosa na akikutwa na hatia atatozwa faini isiyozidi kiasi cha shilingi elfu hamsini au kifungo kisichozidi miezi kumi na miwili au vyote viwili kwa pamoja.

Uteuzi wa Mawakala

12. (1) Halmashauri inaweza kumteua mtu yeyote au kikundi chochote kuwa wakala wa kuikusanyia ada na ushuru chini ya

Sheria Ndogo hizi na mtu yeyote au kikundi kilichoteuliwa kuwa wakala kitakuwa na mamlaka ya kukusanya ada na ushuru kama Halmashauri na kinaweza kutumia mamlaka ya Halmashauri kufungua kesi ya madai Mahakamani dhidi ya mtu yeyote au kikundi chochote kitakachoshindwa kulipa ada na ushuru chini ya Sheria Ndogo hizi kwa taarifa ya awali kwa Halmashauri.

(2) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kubatilisha uteuzi wa wakala pale itakapothibitika baada ya utafiti wa kina kuwa wakala anakiuka masharti ya Sheria Ndogo hizi.

Mamlaka ya kuingia na kukagua

13. Kadri ya masharti ya Sheria Ndogo hizi Afisa yoyote, Wakala au Mwajiriwa wa Halmashauri, atakuwa na mamlaka ya kuingia kwenye ardhi yoyote, jengo lolote, nyumba au chombo chochote ndani ya mamlaka ya Halmashauri kwa lengo la kutekeleza Sheria Ndogo hizi.

Makosa na Adhabu kwa mawakala wa kukusanya ushuru

14. (1) Mtu yeyote, taasisi au kikundi kilichoteuliwa na kupewa jukumu la kukusanya ushuru na bila sababu za msingi,

a) Akishindwa kuleta taarifa za mapato kama zinavoelekezwa na Sheria Ndogo hizi,
b) Akishindwa kurejesha ada na ushuru alivyokusanya baada ya muda wa kuwasilisha kupita,
c) Akishindwa kutunza taarifa zinazohusiana na ada na ushuru zitozwazo na kukusanywa,
d) Atashindwa kutoa taarifa kwa ajiri ya kufanyiwa tathmini na uthamini kadri ya maelekezo ya Sheria,
e) Akizuia au kujaribu kuzuia afisa mwidhiniwa au mkusanya mapato kutekeleza jukumu lake kadri ya mamlaka alinayo katika sheria ndogo hizi,

Atakuwa amefanya kosa na akikutwa na hatia atatozwa faini isiyozidi kiasi cha shilingi elfu hamsini au kifungo kisichozidi miezi kumi na miwili au vyote viwili kwa pamoja.

(2) Pasipo kuathiri maana ya aya ya (1) Halmashauri inaweza kurejesha ada na ushuru uliokusanywa kwa kupitia mashtaka ya jinai na mashauri ya madai.

(3) Mashauri ya madai yatakayofunguliwa mahakamani kuhusiana na madai ya ada na ushuru, yatafunguliwa kwa hati ya mkato (Summary Procedure)

Wajibu wa kutoa taarifa

15. (1) Mtu yeyote atakayetakiwa kutoa taarifa atatoa taarifa hizo kwa utashi wake na kwa kadri atakavyokuwa ametakiwa na Halmashauri kwa ajiri ya kufanya uthamini wa ada na ushuru katika Sheria Ndogo hizi.

(2) Kwa minajiri ya kupata taarifa kama ilivyo katika aya ya (1) ya Sheria Ndogo hizi, Halmshauri inaweza kumtaka mtu yeyote

kufika mbele yake kwa wakati na sehemu itakayoteuliwa.

(3) Mtu yeyote ambaye atakuwa ametakiwa kutoa taarifa katika Sheria Ndogo hizi :-

a) Akikaidi au kukataa bila sababu ya kisheria, au akishindwa kutoa taarifa kama atakavyotakiwa; au
b) Kwa makusudi akapotosha au kujaribu kupotosha Halmashauri katika jambo lolote linalohusiana na ukusanyaji wa ada na ushuru,

Atakuwa amefanya kosa na akikutwa na hatia atatozwa faini isiyozidi kiasi cha shilingi elfu hamsini au kifungo kisichozidi miezi kumi na miwili au vyote viwili kwa pamoja.

Mamlaka ya kukagua

16. Kadri ya Sheria Ndogo hizi, Afisa yeyote au Mwajiriwa wa Halmashauri aliyeidhiniwa kwa maandishi kwa niaba ya Halmashauri anaweza kuingia kwenye ardhi yoyote, jengo, makazi, au chombo ndani ya mamlaka kwa ajiri ya utekelezaji wa sheria ndogo hizi atakagua au kuhitaji utekelezaji wa sheria ndogo hizi.

Makosa na Adhabu

17. (1) Mtu yeyote, ambaye kwa namna yoyote atakuwa na wajibu wa kulipa ada na ushuru katika Sheria Ndogo hizi:-

a) Atapuuza, kukataa, au kushindwa kulipa ada na ushuru kama ilivyooneshwa;
b) Akikwamisha, akishawishi au akisaidia mtu yeyote kutolipa ada na ushuru;
c) Kwa namna yoyote akimzuia Afisa Mwidhiniwa kutekeleza majukumu yake au mamlaka yake katika Sheria Ndogo hizi; au
d) Kwa namna yoyote atakiuka Sheria ndogo hizi;

Atatenda kosa na akikutwa na hatia atatozwa faini isiyozidi kiasi cha shilingi elfu hamsini au kifungo cha miezi kumi na miwili au vyote kwa pamoja na kwa nyogeza ya adhabu hizo atatakiwa kulipia ada au ushuru ambao alipaswa kulipa kwa Halmashauri.

(2) Hakuna lolote katika aya hii litakalochukuliwa kuwa linamhalalishia mtu kinga ya uzembe au kutokuwa na kumbukumbu katika utekelezaji wa majukumu yake katika Sheria ndogo.

Makosa kwa kwa kampuni

18. Pale ambapo makosa yatafanywa na Kampuni na kuthibitika kutenda kosa, kwa ridhaa au ufahamu wa au kuchangiwa na mkurugenzi, meneja, katibu au ofisa yeyote wa kampuni, au mtu yeyote atakayetenda kwa ajiri ya Kampuni, atakuwa anatenda kosa, kampuni pamoja na watendaji wake pale itakapobidi watawajibika.

Kulipwa madeni

19. (1) Malipo yoyote na ada au adhabu vitakavyolipwa na mtu yoyote katika Sheria Ndogo hizi yatakuwa madeni halali yatakayolipwa kwa Halmashauri na yatadaiwa kutoka kwa mtu yeyote kama shauri la madai kwa niaba ya Mkurugenzi au Afisa yeyote aliyeidhiniwa na Mkurugenzi.

(2) Bila kupotosha ujumla wa utaratibu wa mbinu za kurejesha madeni yaliyoelezwa kwenye aya ya (1) hapa juu, pale itakapobainika kuwa mtu anadaiwa na Halmashauri, Mkurugenzi au Afisa yeyote aliyeidhiniwa na mkurugenzi atafungua hati ya madai mahakamani ikieleza kiwango cha kosa na deni linalodaiwa.

(3) Hati iliyowasilishwa mahakamani ikiridhiwa na mahakama yenye mamlaka, itakuwa amri halali ya mahakama dhidi ya mtu anaedaiwa pamoja na riba ya asilimia kumi (10%) tangu tarehe ilipotolewa hadi siku ya kulipwa kwa deni. Amri hiyo itatekelezwa kama zilivyo amri nyingine za mahakama.

(4) Kila hati itakayowasilishwa Mahakamani katika utaratibu ulioelezwa hapa juu, itakuwa ushahidi wa ukweli wa kile kilichooneshwa katika hati hiyo.

Adhabu ya jumla

20. Mtu yeyote atakayekiuka kifungu chochote cha Sheria Ndogo hizi, atakuwa ametenda kosa na iwapo atapatikana na hatia kama hakuna adhabu maalum iliyoainishwa katika kifungu kilichokiukwa atatozwa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini au kifungo kisichopungua miezi sita jela au vyote kwa pamoja, faini na kifungo.

Kufifilisha kosa.

21. Pale mtu yeyote atakapokuwa ametenda kosa, mkurugenzi anaweza kufifilisha kosa hilo na kumuamuru kulipa kiasi atakachoona kinafaa.

## JEDWALI LA KWANZA

### SEHEMU A
### TOZO ZINAZOLIPWA KWA KUKODI MALI ZA HALMASHAURI

*Huduma, Vibali au leseni zinazotolewa* *Ada na Ushuru vinavyotozwa*

**1. MAJENGO YA HALMASHURI:**

a) Ukumbi wa Manispaa …………………………………….……300,000/=
b) Majengo ya makazi……………………………………………Kadri ya mkataba wa pango
c) Majengo ya biashara;

Halmashauri itatoza ushuru wa kupanga vyumba vya sokoni na maeneo mengine kama inavyoonekana hapa chini.

| AINA | ENEO | KIWANGO |
|---|---|---|
| (i) Vyumba | Kirumba sokoni …………………...….200,000/= Kwa Mwezi | |
| (ii) Vyumba | Buzuruga kituo cha mabasi ………..…200,000/= Kwa Mwezi | |
| (iii) Vyumba | Kitangiri…………………….………...80,000/= Kwa Mwezi | |
| (iv) Vyumba | Nyamanoro …………………………...80,000/= Kwa Mwezi | |
| (v) Migahawa | Mwaloni/Kirumba ……………….…...40,000/= Kwa mwezi | |
| (vi) Bucha | Kitangiri, Kirumba, Buzuruga ……..….Kuanzia 30,000/= | |
| (vi) Meza | Soko la Pasiansi, Nyamanaro, Nyakato, Kiloleli, Kitangiri, Kwa Msuka, Ilemela nk, ……………..9,000/= Kwa Mwezi | |

**2. MITAMBO YA UJENZI**

a) Kukodi Grader ……………………………………………850,000/=kwa siku
b) Kukodi Wheel Loader…………………………………....500,000/= kwa siku
c) Kukodi Bulldozer – D8 ………………………………..1,200,000/= kwa siku
d) Kukodi Bulldozer – D4 ………………………………..800,000/= kwa siku
e) Kukodi Cesspit Empire Vehicle………………....…….…200,000/= kwa siku
f) Kukodi medium excavator …………………...…………600,000/= kwa siku
g) Kukodi Dump truck…..……………………..…………1,500,000/= kwa siku

3. **USHURU WA VIWANDA VYA MATOFARI** ................50,000/= Kwa Mwaka

## SEHEMU B
## ADA ZA MATANGAZO

1. Promotion/matangazo ya ukuzaji wa biashara
    a) Matangazo ya asili ya ndani ya Nchi…………………………. .200,000/=
    b) Matangazo kutoka nje ya Nchi …….………Dola za kimarekani 250 kwa tangazo

2. Matangazo ya sanaa mbalimbali
    a) Matangazo ya asili ya ndani ya Nchi …………………………..200,000/=
    b) Matangazo ya asili ya nje ya Nchi …………Dola za kimarekani 150 kwa tangazo

3. Vibali vya mabango ya matangazo……………………….…………….10,000/=
    - $0.1M^2$ hadi $5M^2$ kwa kila ombi……………………………..20,000/=
    - $5.1M^2$ hadi $10M^2$ kwa kila ombi ………………………..…..30,000/=
    - $10.1M^2$ hadi $15M^2$ kwa kila ombi ………………………….40,000/=
    - $15.1M^2$ hadi $20M^2$ kwa kila ombi ………………………….50,000/=
    - $25.1M^2$ hadi $30M^2$ kwa kila ombi ………………………….60,000/=
    - $30.1M^2$ hadi $40M^2$ kwa kila ombi ………………………….70,000/=
    - $40.1M^2$ hadi $50M^2$ kwa kila ombi.………………………….80,000/=
    - $50.1M^2$ hadi $60M^2$ kwa kila ombi ………………………….90,000/=
    - $50.1M^2$ hadi $70M^2$ kwa kila ombi …….…………………...100,000/=
    - $70.1M^2$ na zaidi ……………………….…………………..…...200,000/=

    b) Mabango ya Tri-vision kwa futi za mraba kwa mwaka
        (i) Mabango yasiyong’ara (yasiyowaka) ..…………..………….6,000/=
        (ii) Mabango yanayong’ara (yanayowaka)……....……………..8,000/=
        (iii) Posters (mabango mengineyo)………………………………25/= Kwa siku
        (iv) Banners (ya vitambaa)……….……………………….…..2,000/= (Kwa siku
        (v) PVC ……………….………………………………..…..….8,000/=

    c) Ada ya mabango ya tri-vision ya umeme per sq feet…….. …….15,000/=

4. Matangazo ya Biashara kwa umma (PA)……………………………...200,000/=

---

## SEHEMU C
## ADA ZA MANCHINJIO

a) Ada za kuchinja,
    (i) Ng’ombe ……………………………………………….1,000/=
    (ii) Mbuzi/Kondoo …...…………………………………….500/=
    (iii) Nguruwe ……………………………………………….1000/=

b) Ushuru wa kukagua;
   - (i) Ng'ombe…………………………………………….....1,000/=
   - (ii) Mbuzi/Kondoo….…………………………………...500/=
   - (iii)Nguruwe………..……………………………………1,000/=

c) Ushuru wa mifugo Mnadani
   - (i) Ng'ombe ………………………………………...…3,000/=
   - (ii) Mbuzi/kondoo ………………………………………1,500/=
   - (iii) Nguruwe……………………………………………2,000/=

d) Ada za kuanika ngozi;
   - (i) Ng'ombe………………………………….……....500/=
   - (ii) Mbuzi……….…………………………….……….300/=

e) Ada za awali za kuchunguza wanyama;
   - (i) Ng'ombe ……………………………………………500/=
   - (ii) Mbuzi/Kondoo ...……………………………………200/=
   - (iii)Nguruwe………………………………………..….500/=

f) Ada ya kukusanya na kusafirisha;
   - (i) Ng'ombe ……………………………………………500/=
   - (ii) Mbuzi/Kondoo …………………………...………….300/=

---

## SEHEMU D
## MIFUGO

Ushuru wa mifugo sokoni;
   - (i) Ng'ombe ………………………………….…………..2000/=
   - (ii) Mbuzi/kondoo ………………………………….….500/=
   - (iii)Nguruwe ………………………………….…………...1000/=

---

## SEHEMU E
## USHURU WA SAMAKI NA MAZAO YA ZIWANI

a) Kilo moja ya samaki wabichi ………………………………………30/=

b) Gunia la dagaa kwa vipimo vifuatavyo:
   - (i) Kilo 20 hadi 35………..……………………………...400/=
   - (ii) Kilo 36 hadi 60 ……………………..……………….……700/=
   - (iii) Kilo 61 hadi 100 …………………..….………………1,000/=
   - (iv) Kilo 101 na zaidi.…………………….……..…..……….1,600/=

c) Gunia la konokono la uzito wa kilo 100………….………………...1000/=

d) Samaki wakavu;
   (i) Tenga dogo…………………………………………….…...1,600/=
   (ii) Tenga la kati………………………………….……....…5,000/=
   (iii) Tenga kubwa……………………………………………..…6,000/=

e) Mabondo
   i) Mabondo mabichi……………………………………...1,400/=kwa kilo
   ii) Mabondo makavu…………………………..………………2000/= kwa kilo

f) Dagaa kwa visado viwili 50/=, na kila kinachoongezeka baada ya visado viwili vya kwanza ………………..………..…50/=

---

**SEHEMU F**

**USHURU SOKONI**

**BIDHAA ZILETWAZO NDANI YA MASOKO**

a) Gunia la maharage kuanzia kilo 50 hadi 100……………….……..1,000/=
b) Gunia la Karanga kuanzia kilo 50 hadi 100..…………….………..1,000/=
c) Gunia la ulezi kuanzia kilo 50 hadi 100…………………….…..1,000/=
d) Gunia la viazi vitamu kuanzia kilo 50 hadi 100…..………………..1,000/=
e) Gunia la viazi mviringo kuanzia kilo 50 hadi 100 ………………..1,000/=
f) Gunia la tangawizi kuanzia kilo 50 hadi 100 …...…………………1,000/=
g) Lori la mikungu ya ndizi…………….……………………………..50,000/=
h) Tenga kubwa la nyanya……………………………………………2,000/=
i) Gunia la mahindi kuanzia kilo 100 na zaidi …..………………….…..1,000/=
j) Gunia la mchele kuanzia kilo 100 na zaidi ……………..………....1,000/=
k) Tenga kubwa la kuku…………..…………..………………….....1,500/=
l) Lori la miwa ………………………..…..................................15,000/=
m) Lori la mapapai…………………………………………………..50,000/=
n) Lori la machungwa au maembe …………..……………………..50,000/=
o) Lori la nyanya ……………………………………………………..40,000/=
p) Lori la nanasi………………...…………………………………......50,000/=
q) Lori la tikitimaji……………………..………..........................50,000/=
r) Lori la matango, caroti, matunda ya pasheni……..…………….…..50,000/=
s) Gunia la kabeji……………………………………………..…….2,000/=
t) Gunia la vitunguu……………………………………..………2,000/=

---

**SEHEMU G**

**MAOMBI YA KUKATA BARABARA**

a) Barabara ya lami…
b) Barabara isiyo ya lami………. } Kadri ya tathmini ya Mhandisi

---

**SEHEMU H**
**VITUO VYA KUOSHEA MAGARI**

a) Maeneo muhimu ya Manispaa (katikati ya mji) …………....200,000/= kwa mwezi
b) Nje ya maeneo ya katikati ya mji...…………………………100,000/= kwa mwezi
c) Maeneo mengine....................................................................50,000/= kwa mwezi

---

**SEHEMU I**
**VIBALI VYA UJENZI**

a) Majengo
i) Jengo la makazi la ghorofa moja ……………………..….….….50,000/=
ii) Jengo la makazi la ghorofa mbili ……………………………..…100,000/=
iii) Jengo la makazi zaidi ya ghorofa moja …….. ………………..…500,000/=
iv) Jengo la biashara la ghorofa moja ………………………………100,000/=
v) Jengo la biashara la ghorofa mbili ……………………………....200,000/=
vi) Jengo la biashara ghorofa zaidi ya mbili ………………………...1,000,000/=
Vii) Jengo la biashara………….…………………………………....60,000/=
viii) Taasisi ……..…………………………………………………...200,000/=
xi) Viwanda ………………………………………………………1, 500,000/=
x) Nyumba ya Kawaida ……………………………………..….30, 000/=

c) Kuongeza na kubadili jengo lililopo

| | |
|---|---|
| i). Kwa kuongeza tu | 50% ya kibali cha awali |
| ii) Kwa kubadili | 50% ya kibali cha awali |
| iii) Kuongeza na kubadili | 100% ya kibali cha awali |

---

**SEHEMU J**
**ADA ZA KUNUNUA ZABUNI ZA HALMASHURI**

i) Ukusanyaji wa mapato ………………………………………..…...100,000/=
ii) Ujenzi wa barabara ………………………………………………100, 000/=
iii) Ukusanyaji na uondoshaji wa Taka ngumu……….……………..50,000/=
iv) Kupakua mashimo ya maji machafu (vyoo) ………………..…...100,000/=
v) Kurekebisha na kujenga vyoo vya uma, maduka na vioski...…..…70,000/=

vii) Kurekebisha mali za Halmashauri (magari na majengo)…...........100,000/=
viii) Ukaguzi na upimaji wa viwanja……………………….………......100,000/=
ix) Usimamizi na uendeshaji vyoo vya umma na maduka…………100,000/=
(xi) Uendeshaji na usimamizi wa stalls za Halmashauri………….....50,000/=
(xii) Huduma elekezi / mshauri (Consultancy services) ……..…......100,000/=

---

**SEHEMU K**
**ADA ZA UTHAMINI**

a) Nje ya kituo cha kazi …………………………kadri ya mshahara wa mthamini

---

**SEHEMU L**
**USHURU WA KUGOA VYOMBO VYA USAFIRI VYA MAJINI**

a) Ushuru wa kuegesha vyombo ya usafiri majini……..30,000/= kwa mwaka

---

**SEHEMU M**
**MAZAO YA MALI ASILI**

a) Gunia la mkaa………………………………………….. 1,000/=
b) Mbao, magogo, mirunda
   i) Gari kuanzia tani 1 hadi 2…….……………………..10,000/=
   ii) Gari la kuanzia tani 3 hadi 7……………….……………50, 000/=
   iii) Gari la kuanzia tani 8 hadi 12..………..………..100,000/=
   iv) Gari la kuanzia tani 13 na zaidi………..………..200,000/=

---

**SEHEMU N**
**ADA ZA KUPIMA VIWANJA**

Zitalipwa kadri ya sheria na Kanuni za ardhi na upimaji

---

**SEHEMU O**
**GHARAMA ZA MADINI YA UJENZI**

a) Ada ya Kibali……………………………………..100,000/=kwa heka kwa mwaka
   (i) Mchanga……………….. Gari la Kuanzia tani 3hadi 7 …………..5,000/=
   (ii) Morrram …………………Gari la tani 7 na zaidi ……………… ...10,000/=

(iii) Mawe ………………………Gari la zaidi ya tani7…… …………5,000/=
(iv) Changarawe ……………..Gari la zaidi ya tani 7…………………10,000/=

---

**SEHEMU P**
**MAENEO YA UMMA NA VIWANJA VYA WAZI**
(Bira kuhusisha maeneo yaliyo zuiwa)

Kibali ………………………………………………………………..50,000/=kwa siku

## JEDWALI LA PILI

## FORM OF SUMMARY WARRANT OF ATTACHMENT AND SALE

To the Court Broker
………………………………………..
………………………………………..
………………………………………..

This is to command you to attach and hold the movable/immovable property of …………………………………………………………………………………………… ………………………………………………………………………………… who Shall pay you the sum of Tshs……………………………………………………………… …………………………………. Being the rate due and owing by the said……………………………………………………………………. together with interest at the date……………………………………………………………………… And the cost of this attachment and after giving fourteen days notice by affixing the same to this court house and making due proclamation to sell by auction aforesaid. You are further commanded to return this warrant on or before the ……………………………………………….Day of ……………….. With an endorsement certifying the manner in which it has been executed or reasons why it has not been executed.

Given under my hand and the seal of this Court this…………day of…………20……….……

…………………………………………………………………….
**Resident Magistrate**